

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3  
Fax Na: 2152820  
(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe  
kwa Kamishna Jenerali)



8 Barabara ya Kivukoni,  
S. L. P. 80327,  
**11486 DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KILO 88.27 ZA DAWA ZA KULEVYA ZAKAMATWA JIJINI DAR ES SALAAM**

**Dar es Salaam, 17 Juni, 2021:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), siku ya tarehe 02 Juni 2021 majira ya saa saba usiku katika eneo la Kimara Korogwe mkoani Dar es Salaam, ilifanikiwa kukamata jumla ya Kilo 88.27 za dawa za kulevya aina ya Heroin na Methamphetamine zikiwa ndani ya gari aina ya Toyota Prado likiwa limetelekezwa barabarani.

Dawa hizo zilikamatwa mara baada ya maafisa wa Mamlaka na TRA kulitilia shaka gari hilo na kuanza kulifuatilia. Dereva wa gari baada ya kugundua anafuatiliwa alitelekeza gari na kukimbia.

Baada ya upekuzi wa kisheria kufanyika, ndani ya gari kulipatikana na mifuko mikubwa mitatu aina ya sandarusi (maarufu kama viroba) ndani yake ikiwa na pakti 12 za dawa za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa kilo 12.25 pamoja na kontena za plastiki 73, ndani yake kukiwa na dawa aina ya Methamphetamine zenye uzito wa kilo 76.02. Upelelezi wa shauri hili unaendelea.

Vilevile Mamlaka inapenda kuutaarifu umma kwamba, tarehe 26 Juni kila mwaka, Tanzania huungana na mataifa mengine kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani, ikiwa na lengo la kuongeza uelewa wa jamii na


kuhamasisha Umma kushiriki katika mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Kitaifa maadhimisho yam waka huu yatafanyika Jijini Dodoma katika viwanja vya *Nyerere square* na Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**.

Kauli mbiu ya Mwaka huu inasema "***Tuelimishane juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya, Kuokoa Maisha***". kauli mbiu hii inaelekeza kuwa, jamii inatakiwa kujua ukweli juu ya madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya, ili isijiingize katika matumizi ya dawa hizo. Hatua hiyo itasaidia kuokoa maisha ya watu wengi ambao wangeangamizwa na dawa za kulevya.

Aidha, maadhimisho haya yataanza tarehe 24 Mwezi Juni 2021 na yatatanguliwa na maonesho ya shughuli mbalimbali za udhibiti wa dawa za kulevya zinazofanywa na Taasisi za Serikali, Asasi za kiraia na watu binafsi.

Mamlaka inawaomba wananchi na wakazi wa Dodoma kushiriki kwa wingi katika maadhimisho haya. Pia Mamlaka inapenda kuwakumbusha wataanzania kuendelea kushiriki katika, mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwan yetu sote hivyo tushirikiane katika vita hivi.



Daniel Kasokola

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.**